

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI

01 JUNI, 2026



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI – TAREHE 01 JUNI, 2026

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA FEDHA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

471. MHESHIMIWA JOSHUA SAMWEL NASSARI (ARUMERU MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara kwenye Mji wa Ngarenanyuki kwa kiwango cha lami.

472. MHESHIMIWA DKT. NEEMA PETER MAJULE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha 10% ya fedha za Mapato ya Halmashauri inawafikia Wanawake wa Vijijini.

473. MHESHIMIWA JESCA DAVID KISHOA (IRAMBA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Watumishi katika Zahanati na Vituo vya Afya vilivyopo Wilaya ya Mkalama.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

474. MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA KIKOYO (MULEBA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, lini Serikali itajenga jengo la kisasa la TAKUKURU Wilayani Muleba.

WIZARA YA KILIMO:

475. MHESHIMIWA CHARLES JACOB SUNGURA (HANDENI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itatekeleza ujenzi wa Miradi ya Umwagiliaji katika maeneo ya Masatu, Mumbwi, Kweingoma na Sezakofi.

WIZARA YA UCHUKUZI:

476. MHESHIMIWA SHAFFIN AHMEDALI SUMAR (UYUI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa ajira kwa Vijana na akina Mama wenyeji kwenye ujenzi wa SGR katika Kituo kidogo cha abiria Nzubuka.

477. MHESHIMIWA MARIAM NASSORO KISANGI (TEMEKE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kivuko eneo la SGR - Keko ili kurahisisha Wananchi wa Keko kufika Mjini.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

478. MHESHIMIWA ADO SHAIBU ADO (TUNDURU KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza kwa ukamilifu mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

479. MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali haioni haja ya kugawa hekari chache za eneo la Jeshi la Magereza kwa Wananchi wa Ludewa kwa kuwa kuna upungufu wa Ardhi.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

480. MHESHIMIWA KUNTI YUSUPH MAJALA (CHEMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Majosho katika Wilaya ya Chemba.

481. MHESHIMIWA CLAYTON REVOCATUS CHIPANDO (KIGOMA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia Wavuvi wa Ziwa Tanganyika kwa kuwapatia vifaa vya kisasa, kupunguza tozo na kuboresha teknolojia ya uvuvi.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

482. MHESHIMIWA JAPHAEL MASANJA LUFUNGIJA (ULYANKULU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itatatia migogoro ya mipaka kati ya Wananchi na Hifadhi katika Vijiji vya Mwanduti, Mtwiga, Imagi, Sasu na Mkiligi.

WIZARA YA UJENZI:

483. MHESHIMIWA GEORGE VENANCE LUGOMELA (MASWA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Barabara ya Maswa – Lalago itajengwa kwa kiwango cha lami kama ilivyoahidiwa.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**DODOMA
01 JUNI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE**